
HEAD OFFICE

4th Floor, LAPF House Makole Road
P.O Box 2857, Dodoma, Tanzania

Tel: +255-26 2329002-3; Fax: +255-26 2329005

E-mail: info@ewura.go.tz

Website: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

ONYO KWA MAFUNDI WA KUWEKA MIFUMO YA UMEME

(Limetolewa kwa mujibu wa Ibara 7 (1) ya Sheria ya EWURA namba 414 na Ibara ya 8 ya Sheria ya Umeme namba 131)

TAARIFA inatolewa kwa mafundi wa umeme na umma kwa ujumla kuwa:-

- (a) Ni kosa kisheria kufanya kazi za kuweka mifumo ya umeme (electrical installation) bila kuwa na leseni hai iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA). Hivyo basi, ili kukidhi matakwa ya sheria ya Umeme, kila fundi umeme anayefanya kazi za kuweka mifumo ya umeme, lazima awe na leseni iliyo hai iliyotolewa na EWURA.
- (b) EWURA inatoa tahadhari kwa mafundi umeme wanaotoa huduma za uwekaji wa mifumo ya umeme bila kuwa na leseni halali **kuaacha mara moja** na kuomba leseni EWURA.
- (c) Mafundi wote ambao hawana leseni wanaweza kuomba kutumia mfumo wa kieletroniki wa **Licensing and Ordering Information System** (LOIS) uliopo kwenye Tovuti ya EWURA “www.ewura.go.tz” au kwa kufika Makao Mkuu ya EWURA, Dodoma au ofisi za Kanda za Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Arusha.
- (d) EWURA itafanya ukaguzi endelevu kuwabaini wote watakaondelea kutoa huduma za uwekaji wa mifumo ya umeme bila ya kuwa na leseni, hivyo basi, watachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria. Ili kurahisisha utambuzi, wale wote wenye leseni wanatakiwa kuwa na leseni kila wawapo kazini na wazioneshe pale watakapotakiwa kufanya hivyo na wakaguzi au na wateja wao.

- (e) Wateja wa huduma za uwekaji mifumo ya umeme wanaaswa kuepuka kutumia mafundi wasiokuwa na leseni. Kwa utambuzi ni vyema kuomba kitambulisho cha fundi husika au kutumia orodha ya mafundi inayopatikana kwenye tovuti ya EWURA (www.ewura.go.tz).

**Imetolewa na
Mkurugenzi Mkuu**